Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 7 Juni, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliimba Wimbo wa Taifa)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa hii ya Spika inatolewa chini ya Kanuni ya 33(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007. Katika Mkutano wa Tatu wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada Minne ya Sheria ya Serikali ifuatayo:-

Muswada wa kwanza ni *The Pharmacy Bill* 2010, Muswada wa pili ni *The Economic Zone Laws Miscellaneous Amendments Bill* 2011, Muswada wa tatu ni *The Written Laws Miscellaneous Amendments Bills* 2011, na Muswada wa Nne ni *The Judicial Administration Bill, 2011*.

Mara baada ya kupitishwa na baadaye kupitia katika hatua zake zote za uchapishaji, Miswada hiyo ilipelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili ipate kibali chake. Katika taarifa hii napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba Rais ametoa kibali chake kwa Miswada yote Minne na sasa ni sheria za nchi zinaitwa kama ifuatavyo:-

*The Pharmacy Act 2011*, hii ni sheria namba moja ya mwaka 2011, The *Economic Zone Law Miscellaneous Amendments Act, 2011* hii ni sheria namba mbili ya mwaka 2011. *The Written Laws Miscellaneous Amendment Act 2011* inaitwa sheria namba tatu ya mwaka 2011. *The Judiciary Administration Act*, *2011* nayo imepata namba ya Nne ya mwaka 2011.(*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo katika Bunge hili la Kumi hizo ndizo sheria za kwanza mlizotunga. Kwa hiyo, mna haki ya kujipongeza, tunaendelea na shughuli zingine. (*Makofi*)

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:**

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

### Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Longido

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA (K.n.y. MHE. MICHAEL L. LAIZER)** aliuliza**:-**

Wilaya ya Longido ni miongoni mwa Wilaya mpya ambayo haina Hospitali ya Wilaya lakini tayari Halmashauri wameomba fedha za kujenga hospitali:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nimepata bahati ya kuwa mtu wa kwanza kujibu swali kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Siha nichukue nafasi hii kukupa pole kwa kuondokewa na Mama yako mpendwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya salaam hizo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huduma za afya katika Wilaya ya Longido zinatolewa katika vituo vya Afya vitatu (3) na Zahanati Ishirini (20) zilizopo. Huduma za afya za rufaa hupatikana katika Hospitali ya Mkoa wa Arusha - *Mount Meru Hospital.*

Mheshimiwa Spika, jitihada mbalimbali zimefanyika kuhakikisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Longido unafanyika kama ifuatavyo:-

(i) Halmashauri ya Wilaya ya Longido imetenga eneo la ekari (30) hekta (13) kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

(ii) Halmashauri imepeleka kwa wadau mbalimbali andiko la mradi kwa ajili ya kutafuta vyanzo vingine vya fedha.

(iii) Ramani yenye viwango vinavyotakiwa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya imepatikana.

(iv) Shilingi milioni 900 zilizoombwa mwaka 2010/2011hazikuweza kutolewa na Hazina, lakini Halmashauri inaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha hizo ili kutimiza azma ya kujenga Hospitali hiyo. Katika mwaka 2011/2012, Halmashauri imewasilisha Hazina maombi maalum ya shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali hiyo.

(v) Wananchi wanaendelea kuhamasishwa ili waone umuhimu wa kuchangia ujenzi wa hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kujenga Hospitali ya Wilaya ya Longido hatua kwa hatua kadri fedha zitakavyopatikana.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, ni ahadi ya Serikali ya muda mrefu ikiwemo ahadi ya Bajeti ya mwaka 2010/2011kwamba wananchi wa Longido sasa watapatiwa Hospitali yao ya Wilaya ili waweze kupata matibabu kwa karibu:-

(a)Je, Serikali inawaahidi nini sasa wananchi katika Bajeti hii ya mwaka 2011/2012 ili kuweza kukidhi kiu na tatizo la siku nyingi sana la Wilaya ya Longido.

(b)Iwapo Serikali haitafanikiwa kutenga fedha katika Bajeti hii ya mwaka huu, na kwa kuwa wananchi wa Longido wanatumia kituo cha Afya cha Longido ili kupata matibabu ya Msingi. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuhakikisha kwamba zinapatikana fedha za dharura kwa ajili ya kupanua kituo hicho cha Afya katika mwelekeo wa kupata Hospitali ya Wilaya ili kuweza kuwapatia wananchi huduma hiyo kwa haraka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli na nataka ni-*declare interest* hapa kwamba hii Halmashauri inayozungumzwa ni jirani na Wilaya ya Siha. Kwa hiyo, Hospitali hii ikijengwa

ninahakika pia kwamba wananchi wa Jimbo langu la Siha watanufaika sana na Hospitali hiyo, kwa hiyo sina tatizo sana kulielewa hilo.

Mheshimiwa Spika, nataka tu nikifanye kikao chako hiki na baraza lako hili lielewe kwamba kujenga Hospitali ya Wilaya unahitaji siyo chini ya bilioni tisa, na hivi tunapozungumza hapa sasa kinachotumika ni hivi vituo ambavyo Mheshimiwa Ole Sendeka amevizungumzia kwa ajili ya kuweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza kabisa ambalo nataka nikubaliane naye ni kwamba kuna umuhimu wa Halmashauri yenyewe kuona kwamba inakuwa na mahali ambapo panaitwa kwa muda kwamba hapa ndipo palipo Hospitali ya Wilaya ili mahitaji yote yanayohitajika katika Hospitali ya Wilaya yaweze kupelekwa katika hospitali ile wakati tupo katika kipindi cha mpito kuelekea katika hilo lengo la kuweza kuwa na hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu ukiwa na lengo linakupa mpango na mpango utakupa mkakati na mkakati utakupa mbinu na mbinu zitakupa ushindi kwa maana ya kupatikana kwa hospitali. Ndicho ninachotaka kusema hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili amesema kwamba tusipofanikiwa katika kituo hicho, hiki kituo cha Longido anachokizungumzia hapa pamoja na kile kituo kingine cha kanisa, vituo hivi viwili ni vituo ambavyo vinaweza vikatumika kwa msingi huu anaouzungumza sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, ameuliza kwamba ni shilingi ngapi zimetengwa hapa, naomba nimsomee kwa haraka sana na hili litakuwa ni suala la vipaumbele. Kwa mwaka wa 2010/2011 *Capital Development Grant* ambayo imepelekwa katika Halmashauri hiyo ni shilingi milioni mia mbili na sitini na saba mia tisa na hamsini elfu mia tatu na sitini na hela zilizopelekwa kwa mpango wa MMAM ni shilingi sabini na saba milioni na arobaini na saba elfu.

Sasa hili litakuwa ni suala la vipaumbele vya Halmashauri ya Longido mimi najua kabisa kwamba ni Hospitali ambayo itanisaidia hata katika Halmashauri yangu. Kwa hiyo, mimi nashauri kwamba waangalie uwezekano wa kupeleka hiyo nguvu kubwa ya hizo hela katika hizo hospitali kama anavyosema Mheshimiwa Ole Sendeka. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:**Mheshimiwa Spika ahsante sana. Kwa kuwa Wilaya ya Singida sasa ni Wilaya mbili kwa maana ya Singida Vijijini na Wilaya ya Ikungi na kwa kuwa Hospitali Teule ya Makyungu sasa inahudumia Wilaya ya Ikungi.

Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuiteua hospitali ya Kijota ili iweze kuwa hospitali teule kwa Wilaya ya Singida Vijijini?

**SPIKA**: Mheshimiwa Naibu Waziri ingawa ni swali jipya kabisa hili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, suala la kuwa na hospitali ya Wilaya ambayo inaitwa *DDH* kwa maana ya *Designated District Hospital* wala halina mjadala kwa sababu ni suala ambalo ki-*policy* limeshakubalika. Wanachotakiwa wenzetu wa Singida ni wao kuonesha kwamba kuna hitaji hilo la kuwa na hospitali teule, na wakishatamka hivyo wala hakuna tatizo, unaweza ukawa na hospitali ya Wilaya lakini ukawa na hospitali teule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama Mheshimiwa Chilolo anaona kwamba kuna umuhimu wa kufanya hivyo ni suala la kuliweka katika mipango ili tuweze kuingiza katika mipango ya Wizara na tuweze kusaidiana na Halmashauri, sioni tatizo lolote katika jambo hilo. (*Makofi*)

Na. 2

**Uvamizi wa Maeneo ya Shule kwa Shughuli Nyingine**

**MHE. LETICIA M. NYERERE (K.n.y. MHE. RACHEL R. MASHISHANGA)** aliuliza:-

Serikali imeweka sera na Kanuni za kutoruhusu maeneo ya shule kujengwa au kutolewa kwa wawekezaji kwa ajili ya biashara lakini licha ya Kanuni na taratibu hizo, baadhi ya Halmashauri huuza maeneo au viwanja kwa Wawekezaji ili wajenge maduka kinyume na Kanuni za utoaji wa elimu:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha utulivu na usalama katika shule za wasichana za Uhuru na Kibasila.

(b)Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa vibanda vya biashara vilivyojengwa kwenye maeneo ya shule katika Halmashauri mbalimbali nchini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali ina taarifa ya kuwepo kwa ujenzi usiozingatia kanuni na taratibu uliofanyika katika baadhi ya shule hapa nchini. Hali hii inatokana na ukiukwaji wa sheria, taratibu na Kanuni za ujenzi uliofanyika na hivyo kuathiri hali ya utulivu na usalama katika maeneo ya shule husika.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua tatizo hili Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa pamoja ilitoa maelekezo kwa nyakati tofauti kuzuia vibanda vya biashara kujengwa kwenye maeneo ya shule.

Mheshimiwa Spika, baada ya Halmashauri zetu kupokea agizo hili, Halmashauri kupokea agizo hili, Halmashauri zilitekeleza yafuatayo:-

(i) Kutoruhusu mikataba mipya kuendelea kufanyika; mfano kukataliwa kwa maombi ya Wasini *Shopping Centre* na Msikimwe *Company Limited* za Dar es Salaam kuwekeza katika shule ya msingi Uhuru Wasichana.

(ii) Halmashauri zimeagiza kwa Wafanyabiashara wenye vibanda katika maeneo ya shule kusitisha kuendelea na biashara kwenye maeneo hayo.

(iii) Halmashauri kuvunja vibanda vya biashara vilivyoanza kujengwa kinyume na na sheria katika shule ya Sekondari kwa mfano Manzese. Vibanda hivyo vilivunjwa na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala na imepanga kujenga uzio usiokuwa na vibanda vya Maduka. Mkoa wa Mwanza pia walishachukua hatua kama hizo.

(iv) Kibanda kilichopo Kibasila Sekondari ni kantini inayowahudumia watumishi, walimu na wanafunzi pekee na kipo ndani ya uzio.

(b) Mheshimiwa Spika, OWM-TAMISEMI inaendelea kufuatilia hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika usitishaji wa matumizi ya maeneo ya shule kinyume na utaratibu. Kwa kuwa mpango huu ni wa Serikali tunawaomba Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani popote walipo, wakishirikiana na wananchi wasimamie utekelezaji wa agizo hili ili kurudisha nidhamu na utulivu katika maeneo ya shule. Mamlaka zote zizingatie sheria na Kanuni za Mipango Miji.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa tatizo hili limekuwa likiendelea bila kukoma.

Je, Serikali inatoa adhabu gani kwa Wakurugenzi husika ambao wanaendelea kukiuka sheria na kuuza maeneo ambayo ni muhimu kwa matumizi ya wananchi?

Je kuna kifungu au nini pengine labda Serikali inatakiwa sasa iweke adhabu ambayo itatusaidia kukomesha tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwanza pamoja na hatua tulizozichukua kwa kuagiza Halmashauri zote kudhibiti ujenzi holela wa vibanda kwenye maeneo ya shule, tumeagiza kuunda timu za kupitia mikataba yote ambayo inaendelea kujengwa kwenye maeneo yetu ya shule.

Lakini jambo la pili Kamati zile ndizo ambazo zinaangalia, kwanza tumesitisha lakini pia wataangalia kama kuna mkataba wowote ambao unaendelea lakini jibu la msingi limeeleza kwamba tumezuia ujenzi wa vibanda holela kwenye maeneo ya shule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hatutegemei sana kama kutakuwa na ujenzi huo na Wakurugenzi ndiyo wakuu wa zile timu.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ajibu swali langu, ninaomba kujua adhabu gani inatolewa kwa hao wanaokiuka, nimeuliza. Je, Kuna utaratibu wa kuwapeleka jela, kuwatoza faini au kuna adhabu gani ambayo inatolewa.

**SPIKA**: Mheshimiwa Leticia, hatuna utaratibu wa namna hiyo, uliuliza swali la msingi, ukapewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na kama hukuridhika hautumii utaratibu kama ulivyofanya. Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara Nishati na Madini.

Na. 3

**Vyanzo vya Kuzalisha Umeme wa Kutosheleza Mahitaji ya Nchi.**

**MHE. BETTY E. MACHANGU** aliuliza:-

Kwa mujibu wa taarifa kutoka RUBADA iko miradi saba (7) inayoweza kuzalisha umeme wa kutosha mahitaji ya nchi na ziada ambayo ni mradi wa *Stigler's* wenye uwezo wa kuzalisha MW 2,100, gharama ya mradi dola bilioni 2, Wawekezaji kutoka Afrika Kusini; mradi wa Mpanga MW165 gharama yake dola milioni 175; mradi wa Mto Mnyera MW 485, miradi mingine ni Ruhuji, Lukose, Iringa na Kilombero yote katika Bonde la Mto Rufiji, na kama miradi yote saba itatekelezwa ingezalisha MW 3456 ambazo zinatosha kwa matumizi yote ya nchi na ziada:-

(a)Je, Serikali inaweza kuwaeleza Watanzania sababu za kutoitekeleza miradi hiyo ili kuondokana kabisa na tatizo la umeme?

(b)Je, Serikali haioni kuwa inatumia fedha nyingi kulipa *IPTL,* SONGAS na AGRECO badala yake ingetekeleza miradi iliyotajwa kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Betty Machangu, Mbunge wa Viti Maalum. lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa miradi katika sekta ya umeme unaongozwa na mpango kabambe wa uendelezaji wa sekta ya umeme *(Power System Master Plan-*

*PSMP)* ambao hufanyiwa durusu mara kwa mara kulingana na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii.

Miradi iliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge iliyopo katika Bonde la Rufiji na *Stigler's Gorge* (MW 2,100), Mpango (MW 165), Ruhuji (MW 358), Rumakali (MW 222), Lukose na Masigira (MW118) imefanyiwa tathmini wakati wa kutayarisha *Power Sector Master Plan* mwaka 2008 na iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. *(Makofi)*

(b)Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutumia makampuni binafsi ya uzalishaji wa umeme yaani *Independent power Producers* kama yalivyo mampuni ya *SONGAS, IPTL* na AGGREKO ni utaratibu wa kawaida wa Serikali mbali mbali Duniani wa kushirikisha sekta binafsi katika uzalishaji wa umeme.

Katika kipindi hiki ambacho nchi yetu imekumbwa na upungufu mkubwa wa umeme kwenye mfumo wa gridi, vituo vya Songas na IPTL vimekuwa mchango mkubwa katika kupunguza athari za uzalishaji wa umeme usiokidhi mahitaji yanayokua ya umeme nchini.

Miradi hii ni mkakati yenye muda maalum kulingana na makubaliano na mikataba iliyoafikiwa ya kuondoa tatizo la umeme nchini na miradi kama ile aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ni mikakati ya muda mrefu, kwa kuwa inakuwa chini ya umiliki wa umma.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa kununua umeme kutoka kampuni ya AGGREKO ambao ulikuwa wa MW 40 ulimalizika mwaka 2007.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, ziko *mission* zinatengeneza umeme katika maeneo yao kwa mfano kule Tosamaganga wako Wamissionary wanatengeneza KW 1200 kule Mbalizi KW 340, kule Kukiletwa Moshi 1160, Ngarasero Arusha na kule Soni Lushoto.

(a)Ili kutimiza azma ya *REA (Rural electrification* Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuunga mkono na kuhamasisha wananchi wabunifu ili wajitengenezee umeme katika maeneo yao?

(b)Je, ni kwa kiasi gani watalaam ambao siyo wafanyakazi wa *TANESCO* wanahusishwa katika suala la kufufua umeme nchini Tanzania? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hii miradi aliyoitaja iko kwenye *classification* ya *mean hydrous*. Ametaja Kikuletwa, ametaja Tosamaganga ametaja Mbalizi, kwa mfano huu wa Kikiletwa na Tosamanganga ni miradi ya zamani nadhani hii ni miradi ya tangu 1950s huko.

Kwa hiyo, wakati huo kwa maana upatikanaji wa maji ulikuwa mkubwa kidogo zaidi kwenye vituo hivi na uzalishaji wake mahitaji yake yalikuwa siyo makubwa. Sasa swali ameuliza amesema kama Serikali inaunga mkono kupitia *REA* miradi hii, naomba

nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sababu ya kuundwa REA ni hiyo kwamba siyo tu iunganishwe umeme kwenye maeneo ya vijijini Tanzania lakini pia ifanye mikakati ya makusudi ya kuunga mkono miradi inayoibuliwa kama hii ya Kikuletwa na Tosamaganga na iko mingine mingi, iko Mbalizi kuna maporomoko ya maji Nzovwe kule maeneo ya Rukwa kuna maporomoko ya Maporomoko ya Namtumbo. Maeneo yote haya yanashughulikiwa na REA kuangalia namna ambavyo yanaweza kuibuliwa ili kwa maeneo yale *out of grid* miradi hii midogo midogo ya umeme iweze ikachangia upatikanaji wa nishati hiyo kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, la watalaam waliokuwa nje ya *TANESCO* kuchangia katika upatikanaji wa umeme katika suala hili lote la kutatua tatizo la umeme nchini tuna watalaam walioko *TANESCO*, tuna watalaam walioko EWURA, tuna watalaam walioko Wizarani, kwa hiyo, fikra iliyopo ni kwamba sisi wote kwa pamoja tuchangie katika utekelezaji kupata ufanisi wa miradi hii iliyoibuliwa na Serikali lakini pia kama kuna uwezekano ambao watalaam wamebuni miradi yenyewe iko miradi mbalimbali ambayo inapitia huko huko *REA* ya kuwapa motisha hawa wanaobuni vyanzo mbalimbali vya nishati na wanapewa motisha za aina mbalimbali ili kuweza kuchangia na wao katika jambo hili ambalo linatuhusu wote. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. MOSES JOSEPH MACHALI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini katika Bunge la Februari iliahidi kuwa miradi ya umeme iliyopo katika Wilaya za Kasulu pamoja na Kibondo kwamba umeme wake ingekamilika ndani ya mwezi Machi na umeme ungewaka kuanzia mwezi Machi lakini mpaka leo umeme haujaweza kuwaka katika Wilaya hizo na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikifanya naye mawasiliano akini amekuwa akiniambia kwamba tatizo limekuwa ni nyaya ambazo hazikuwepo hapa nchini walikuwa wameagiza nyaya kutoka nje na hatimaye ziweze kupelekwa katika miradi hiyo.

Je, Waziri anawaeleza nini wananchi wa Wilaya za Kibondo pamoja Kasulu umeme huu utawaka *exactly* lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tatizo la upatikanaji wa nyaya kama ilivyo vifaa vingine vinavyoagizwa nje ni tatizo ambalo limeisumbua *TANESCO* kwa muda wa kama miezi tisa (9) au mwaka uliopita. Kwa hiyo, kama *TANESCO* walikuwa wamekadiria kama Machi 2011 wangekuwa wamekamilisha mimi naomba nimwahidi kwamba Kibondo na Kasulu ni miradi ambayo ilikuwepo pamoja na miradi ile ya Longido na miradi ile ya Rukwa ya majenereta. Utaratibu wake wa kukamilika ulikuwa umeshakadiriwa kufikia Machi 2011.

Sasa mimi naomba niwahakikishie wananchi wa Kibondo na wananchi wa Kasulu kwamba mimi na Mheshimiwa Mbunge, tutawasiliana na watu wa *TANESCO* ili tupate kwa uhakika kabisa kwamba upatikanaji wa hizi nyaya zitapatikana lini na naomba nimhakikishie kwamba kwa sababu ni miradi iliyochelewa pamoja na ile mingine yote itapewa kipaumbele katika utekelezaji wake.

Na. 4

**Tatizo la Umeme Nchini**

**MHE. DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALLA** aliuliza:-

(a) Tangu Serikali ya Awamu ya Pili hadi leo Serikali imetumia jumla ya shilingi ngapi kuzalisha umeme na bado tatizo lipo?

(b) Je, tatizo la umeme nchini litaisha lini?

(c) Kwa nini Serikali inaongeza mipango mingi ya kutatua tatizo la umeme bila kutekeleza na kwa nini suala la upatikanaji umeme nchini ni la dharura kila siku?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa Serikali katika miradi ya kuzalisha umeme tangu kipindi cha Serikali ya awamu ya pili hadi leo unafikia jumla ya dola za Marekani milioni 798.

(b) Mheshimiwa Spika, tatizo la uhaba wa umeme litaisha baada ya kutekeleza kwa ukamilifu na kwa wakati mpango wa kipindi kifupi cha mwaka 2011 – 2015 kama ilivyofafanuliwa kwenye mpango kabambe wa uendelezaji wa sekta ya umeme wa mwaka 2008 *Power Sector Master Plan*. Miradi itakayotekelezwa kipindi hicho itaongeza jumla ya MW 1830 kwenye mfumo wa gridi ya taifa. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mepesi mepesi ya Waziri naomba kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kama Serikali iliwekeza kutoka Awamu ya Pili mpaka leo jumla ya dola za Kimarekani milioni 798 itatoa wapi milioni 3700 katika kipindi cha miaka minne ambayo imeelezwa katika jibu?

(b)Kama miundombinu ya kutoa gas Mnazibay kuleta Dar es Salaam tayari imeshakuwa *exhausted* mpaka leo hii Serikali inatuhakikishia vipi tatizo la umeme litapatiwa ufumbuzi wa haraka na siyo kuwa kila siku mgao na dharura? (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imeazimia kutekeleza kwa wakati miradi ya kuzalisha na kusafirisha umeme kulingana na mpango kabambe *PSMP* katika kipindi cha mwaka 2011 – 2018. Miradi iliyopangwa kujengwa itaongeza MW 600 kwa kutumia

maporomoko ya nguvu za maji, MW 870 kwa kutumia gesi asilia, MW 1200 kwa kutumia makaa ya mawe na MW 100 kwa kutumia nguvu ya upepo. Serikali inategemea miradi hii itakamilika kwa kushirikisha uwekezaji wa sekta binafsi kwa kuwa gharama za miradi hii yote ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeanza mikakati ya kutafuta fedha za kugharimia miradi ya kipaumbele niliyoitaja hajo juu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kigwangalla ameuliza swali ya kwamba kutoka Awamu ya Pili mpaka sasa ni miradi gani imepata uwekezaji kwa kiasi gani? Nimemwambia ni US dola milioni 798 sasa anauliza kwa miradi hii mikubwa mingine fedha zitatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimfahamishe tu Mheshimiwa Hamisi Kigwangalla kwamba yale majibu niliyokuwa nampa siyo majibu mepesi mepesi. Mwaka 1985 mahitaji ya umeme ya Tanzania yalikuwa tofauti na mwaka 2011. Uchumi unakua katika kiwango tofauti na uchumi unavyokua ndio mahitaji ya umeme yanavyokua.

Kwa hiyo, sasa hivi mahitaji ya umeme yanakuwa kwa asilimia 13. Kwa mfano tuliokuwa nao sasa hivi tukiongeza uwezo wa usambazaji yatakua zaidi kwa sababu Watanzania wengi wanahitaji nishati hii ya umeme. Ndio maana kwenye Bajeti ya mwaka huu tumekubaliana kwamba kipaumbele kitakuwa ni suala la umeme kwa kujua kwamba suala la umeme ni mchango wazi kabisa katika maendeleo ya Watanzania. Sasa nadhani kwenye majibu yangu pia nimemwamba Dkt. Hamisi kwamba lazima tushirikishe sekta binafsi. Hilo limewezeshwa na sheria ya umeme ya mwaka 2008 ambalo limepitishwa na Bunge lako Tukufu.

Kwa hiyo, nimesema kwamba Serikali inafanya utaratibu wa makusudi ili kushirikisha sekta ya umeme katika utekelezaji wa miradi hii ni mikubwa, gharama zake ni kubwa lakini maendeleo na hali ya uchumi wa Tanzania sasa hivi imetuwezesha kwamba tuna *credit rate* kubwa zaidi. Kwa hiyo, uwezo wetu wa kukopesheka kama nchi ni mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba katika hayo malengo yatafikiwa kwa sababu kwanza katika miaka hii mitano ni megawati 870 na ninaamini kwamba imeshapata wawekezaji binafsi katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika swali hili la pili amesema tutafanyaje kuhusu umeme wa Mnazi Bay ambao miundombinu yake kuja kutoka Mnazi Bay mpaka Dar es Salaam imeshachakaa. Naomba nimsaidie Mheshimiwa Mbunge hakuna miundombinu ya kutoka Mnazi Bay kuja Dar es Salaam. Kwa hiyo, taarifa hiyo kidogo iko pembeni.

Miundombinu inayotoka Mnazibay inakwenda kwenye kituo cha kuzalisha umeme Mtwara Mjini ambayo inazalisha umeme kwa ajili ya mradi wa *Mtwara Electricity Program* ambayo inahudumia Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mradi uliopo sasa hivi ni wa kuwa na bomba la *gas* asilia la kutoa umeme kutoka Mtwara Mnazibay pale mpaka Dar es Salaam cha kiwango cha nchi 30 ili mahitaji yote ya gas njiani kuanzia Somanga MW 300 mpaka Dar es Salaam lakini pia kutumia gasi kwa ajili ya matumizi mengine ikiwa ni gas ya nyumbani yapatikane, sasa mradi huo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameanza kuushughulikia na sisi ni matarajio yetu kwamba hizo njia ambazo zitawezesha kupatikana fedha za mradi huo ambao ni kama dola milioni 570 kama shilingi za Tanzania bilioni 900 zitapatikana na tunatakiwa sisi Watanzania tuwekeze hela kidogo kama asilimia 15, asilimia 20 na zingine mwekezaji ataweka. Lakini tunataka mradi huu ubaki katika mikono ya Watanzania ili iweze kuwa na manufaa zaidi kwa wananchi wa nchi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu mepesi mepesi sasa yamepata uzito.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la umeme limekuwa tatizo sugu hapa nchini na hivi karibuni Serikali ilikuwa imetangaza mgao wa umeme na baadaye wakasema mgao wa umeme umekwisha. Lakini bado kulikuwa na *contradiction* kuna maeneo mengine yalikuwa hayana umeme.

Je, Waziri anaweza akatoa tamko rasmi ili Watanzania wajue kuwa umeme upo au umeisha maana tumekuwa tukipewa orodha ya miradi ya umeme lakini tatizo liko pale pale? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tukubaliane tu tatizo la umeme sasa hata hii mitambo inayofanyakazi ikiwa inafanya kazi yote bado tuna *deficit* ya *megawatt* 260. Kwa hiyo, ukisema kwamba mgao umekwisha haiwezekani tuna nakisi ya MW 260 wakati wa matumizi ya juu ya *peak*.

Sasa tulichosema ni kwamba upatikanaji ule wa umeme wa mitambo ile tuliyokuwa nayo wakati ule mitambo ilikuwa na matatizo nadhani mwezi wa 12 vile vinu vinavyokwenda kule Songosongo viwili vilipata matatizo tukavizuia tukavisimamisha na juzi hapa mwezi wa tano upatikanaji wa Songosongo ulisimama ili kufanya matengenezo *routine maintenance*, lakini *maintenance* kubwa kwenye mitambo ya Songosongo ili iweze kuendelea kuwa insurable yaani iweze kupata vinginevyo hakuna mtu wa kutoa bima pale. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, kwa hiyo, ninachomwomba Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwamba waelewe kwamba nakisi ni MW 260 ndio maana mwezi wa pili tukasema tutaingiza umeme wa dharura wa MW 260 kwa bahati nzuri Symbion wameleta MW kama 110.

Sasa hivi kwa maana ya umeme wa dharura utakuwa kama MW 30 tunatarajia mpaka mwisho wa mwezi wa 7 au mwanzo wa mwezi wa 8 miradi hii itakuwa imeondoka na tutapunguza tatizo la umeme hasa ikizingatiwa kwamba mahitaji yanakua kwa asilimia 13 kila mwaka.

Na. 5

**Vocha za Pembejeo**

**MHE. SAID AMOUR ARFI (K.n.y. MHE. DAVID ERNEST E. SILINDE)** aliuliza:-

Sera ya Kilimo Kwanza inalenga kumkomboa Mtanzania kutoka kwenye umaskini kupitia kilimo lakini pia ni kuinua uchumi wa nchi:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kutumia utaratibu wa vocha kuwafikishia pembejeo wakulima, uteuzi wa wakulima walengwa unafanywa kwa majina ya wakulima kuidhinishwa na mkutano mkuu wa Kijiji. Wakulima ambao wameidhinishwa huwa na haki ya kudai kupata ruzuku hiyo wasipoipata. Utaratibu huu ukifuatwa vizuri, matarajio yetu ni kwamba walengwa watanufaika. Pale utaratibu huu unapokiukwa walengwa hawanufaiki.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kusimamia utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa utaratibu wa vocha hatua mbalimbali zimechukuliwa dhidi ya wanaokiuka kwa mfano katika msimu wa 2009/2010 jumla ya kesi 22 zilifunguliwa mahakamani katika Mikoa ya Rukwa kesi (2) Mwanza kesi (3), Mara kesi (4), Morogoro kesi (3), Manyara kesi (2) Kilimanjaro kesi (2) Iringa kesi (1) na Mbeya kesi (5).

Pia baadhi ya mawakala waliobainika kudanganya tayari wamefutiwa ridhaa hiyo ya kusambaza pembejeo kwa wakulima katika msimu wa 2010/2011 katika Mikoa ya Morogoro mawakala walifutiwa (6) Mkoa Rukwa (116) wanaongoza hao. Mkoa wa Mbeya (13) na Ruvuma (39).

(c) Mheshimiwa Spika, mfumo wa ugawaji wa vocha za pembejeo za kilimo uliopo kwa sasa unaonekana ni mzuri zaidi ukilinganisha na mfumo wa zamani ambapo Serikali iliingia mikataba na makampuni binafsi ya pembejeo za kilimo ili kusambaza pembejeo hizo kwa wakulima. Vocha kwa utaratibu huu wa sasa zinafika hadi vijijini na kugawiwa kwa wakulima walengwa kupitia Kamati za Vocha. Aidha, wauza pembejeo kwa sasa wanalazimika kufikisha pembejeo za kilimo hadi vijijini ambako wanunuzi wanapatikana, ukilinganishwa na wakulima kufuata pembejeo Wilayani kabla ya utaratibu huu kuanza katika msimu wa 2010/2011.

Katika msimu wa 2010/2011 jumla ya wakulima 2,000,000 wamenufaika na ruzuku ya pembejeo kwa mazao ya chakula na wakulima takribani 600,000 wamenufaika na zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, upungufu unaojitokeza kwa sasa ni kutokana na usimamizi hafifu katika ngazi husika za Kamati za Vocha. Ili kuhakikisha kwamba tatizo hili linapatiwa ufumbuzi Wizara yangu inasisitiza kwamba Kamati za Vocha za Wilaya, Kata na Vijiji zizingatie maendeleo yaliyotolewa katika waraka wa usimamizi wa utekelezaji yaliyotolewa katika waraka wa usimamizi wa utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa utaratibu wa vocha wa msimu wa 2011/2011.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusisitiza juu ya usimamizi makini wa utaratibu wa vocha katika msimu wa 2010/2011. Aidha, Serikali imemwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum *(Special Audit)* kwenye maeneo mbalimbali ambako utaratibu huu unatekelezwa na wale watakaobainika kuhujumu utaratibu huu watachukuliwa hatua za kisheria na kinidhamu kulingana na makosa yao.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushuru ninayo maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba mfumo huo wa ugawaji wa pembejeo za kilimo uliopo sasa unaonekana ni mzuri. Lakini malamiko ni mengi sasa sijui huo uzuri ni wapi kama Rukwa tu pekee yake kuna mawakala zaidi ya 116 kama alivyoeleza, lakini pia kwa sababu katika Mikoa ambayo kumekuwa na usambazaji wa *voucher* yamekuwepo malalamiko mengi sasa:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kama inavyosema kufanya *special audit* katika maeneo yote na sio maeneo maalum?

(b) Swali la pili, kwa kuwa mawakala walisambaza pembejeo na hawajalipwa fedha zao, kuna mpango gani wa kuwalipa fedha zao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Arfi, kama ifuatavyo:-

Ni kweli malalamiko yako mengi, lakini kama tunavyojua utaratibu unapoanza lazima katika utekelezaji kuna kukwama hapa na pale. Lakini sisi tathmini tulikwisha ifanya inaonyesha kwamba mwaka hadi mwaka kuna mabadiliko, kuna mafanikio yanajitokeza na utaratibu huu sio kwamba ni wa kudumu maana haitawezekana wakulima wote wa Tanzania tuwape mbolea kama wanavyotarajia, tunataria kwamba tukifika mahali tunajenga uwezo tu wa wakulima kujitegemea wenyewe.

Kwa mfano wale wakulima wa mwanzo laki saba tulioanza nao, baada ya msimu huu hawatakuwemo katika utaratibu huu, tunaanza na wengine. Lengo ni kwamba tuwajengee uwezo hatimaye wa kujijengea uwezo wa kununua mbolea wenyewe. Lakini nikija kwenye majibu halisi ni kwamba *special audit* niliyoisema si kwa ajili ya maeneo tu machache tu niliyosema, tumemwomba CAG akaguwe maana yake utaratibu huu tumeupanua katika nchi nzima. Kwa hiyo, tutafanya *special audit* sehemu zote ambazo utaratibu huu umetumika. Kuhusu wale mawakala ambao hawajalipwa ni kweli na mimi

mwenyewe nimepata malalamiko mengi sana, lakini nataka nimhakikishie kwamba Wizara ya Fedha sasa inafanya utaratibu, tunashirikiana tuhakikishe kwamba mawakala wote ambao hawajalipwa wanalipwa mafao yao.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mfumo huu wa *vouche*r kwa hakika umeisaidia sana nchi yetu ya Tanzania kuondokana na tatizo la njaa kwa kuwa ile Mikoa inayozalisha chakula imeweza kuzalisha chakula mara mbili zaidi. Lakini kwa kuwa sababu pia za kiutaalam zinaeleza wazi kadiri unavyoweka mbolea ya kutosha kwenye udongo ndivyo unavyozalisha zaidi na zaidi na kwa kuwa voucher ya mfuko wa kukuzia kwenye mpango wa voucher inaruhusu upatikanaji wa mfuko mmoja kwa hekari moja badala ya mifuko miwili ambayo kwa kweli kiutalamu ndiyo inayotosheleza kurutubisha ardhi?

Je, Serikali sasa iko tayari katika mfumo huo huo kuongeza utaratibu wa kupata mifuko miwili ya *voucher* ya kukuzia ili kuongeza uzalishaji na kuondoa kabisa tatizo la njaa katika nchi yetu, katika Mikoa ile ambayo inalima chakula kwa wingi na kunusuru Taifa letu na balaa la njaa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mhagama na kwamba kwanza nimpongeze kabisa kwa sababu katika eneo lake, matokeo ya matumizi ya mbolea ni mazuri, inaonekana wameitikia vizuri na kwa sababu hiyo tuna sababu zote za kuangalia pale ambapo kuna mafanikio basi hapo ndipo tunapochukua *model* ili tuweze kuendeleza mahali pengine.

Ushauri wake mimi niseme nimeuchukua, tutaupeleka pale katika Wizara, wataalam wataenda tena kule hasa katika Jimbo lake na nadhani kumetokea mambo mazuri zaidi ili tuangalie, halafu *model* hiyo tutaangalia kama inafaa tuweze kuitumia pia kwa Watanzania wengine.

Na. 6

**Maji kwa Wakulima Wanaopakana na Mashamba ya Kapunga NAFCO - Mbarali**

**MHE. MODESTUS D. KILUFI** aliuliza:-

(a) Je, Serikali imeweka utaratibu gani wa kuwasaidia wakulima wanaopakana na Mashamba ya Kapunga Chimala na *NAFCO* ambayo awali yalikuwa yanamilikiwa na Serikali waliruhusiwa kutumia matoleo ya maji baada ya kutumika na kisha kutiririka kwenye mto Ruaha?

(b)Je, Serikali iko tayari kuruhusu wananchi kuendelea kutumia mabanio madogo madogo ambayo yalivunjwa kwenye maeneo ya Mwashikamile na Yala kwa ajili ya umwagiliaji kwenye mashamba yao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mbunge wa Mbarali, lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya usimamizi wa Rasilimali za maji namba 11 ya mwaka 2009 inawatakia watumiaji wa maji kurudisha maji ya matoleo kwenye mkondo wa mto baada ya matumizi yaliyolengwa. Wakulima wanaopakana na mashamba ya mpunga ya Kapunga na Mbarali yaliyokuwa yanamilikiwa na Shirika la *NAFCO* walianza kutumia maji matoleo baada ya kuona faida zinazotokana na kilimo cha umwagiliaji. Baada ya kubainika kuwa maji yalikuwa yanatumika kinyume cha sheria, Serikali kupitia Bodi ya Mto Rufiji ilizuia matumizi ya maji hayo.

Mheshimiwa Spika, Ili kuwasaidia wakulima waliokuwa wanatumia maji ya matoleo kutoka katika shamba la Mbarali, Serikali imeamua sasa kuendeleza skimu ya umwagiliaji ya mwendamtitu katika mwaka wa fedha 2011/2012 kwa ajili ya wakumima wanaotoka katika Vijiji vya Mwakaganga, Mwanavala, Nyeregete, Urunda, Ibumila, Imalilo, Usongwe na Utyego.

Mheshimiwa Mbunge niwie radhi kama kuna maneno nimetamka visivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maeneo ya Mwashikamile na Yala yako karibu na mbuga ya wanyama ya Ruaha, hata kama kungekuwa na chanzo kingine cha maji isingekuwa busara kuendeleza kilimo katika maeneo hayo kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za usalama wa wanyama, wakulima na mazao yao.

Nawashauri wakulima kutumia skimu za umwagiliaji za Lyanyula, Uturo, Mpolo, Mbuyuni na Ruanda Majenje ambazo tayari zimeboreshwa. Aidha, skimu nyingine zinatarajiwa kuongezeka baada ya ujenzi wa Bwawa la lwanyo kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, kuruhusu wananchi kuendelea kutumia mabanio ya Mwashikamile na Yala itakuwa ni kwenda kinyume na Sheria ile Namba 11 ya mwaka 2009. Napenda kutumia fursa hii kuitaka Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kuhakikisha kwamba wakulima wanapata maeneo ya kulima katika skimu hizo ambazo nimezitaja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina maswali ya nyongeza yenye sehemu a, b na c kwa vile shamba la *NAFCO* Mbarali linapoanzishwa Mheshimiwa Rais wa kwanza Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kutumia wataalamu alishawishi wachina walipokuwa wanaanda shamba lile, waweke matoleo kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wadogo wanalolizunguka shamba na wataalamu walifanya kazi hiyo na wananchi hao wamekuwa wakineemeka na huduma hiyo nzuri kwa maana ya kuendeleza kilimo kwa kwa wananchi wanaozunguka shamba lile:-

(a) Je, kwa maelezo haya Mheshimiwa Waziri anataka kuniambia kwamba mpango huo mzuri ulioandaliwa na Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere kwamba sasa haupo tena?

(b) Kwa vile maeneo ya Mwashikamire na Yala, Mheshimiwa Waziri kwa mara ya kwanza nayatamka hapa Bungeni kwamba yapo karibu na hifadhi mimi ndiyo nasikia, nina hakika kabisa kwamba maeneo yote yanayozunguka hifadhi ya Taifa wananchi walishahamishwa hawapo tena. Sasa taarifa hii ya maeneo hayo kuingizwa kwenye hifadhi hata mimi sijui na wananchi wa maeneo yale hawajui, nataka anihakikishie ni lini maeneo hayo yameingizwa kwenye hifadhi?

**SPIKA:** Hakuna C mheshimiwa ni a,b basi. Kanuni zinakataa. Unasikia Mheshimiwa Mbunge kaa chini. Kanuni zetu zinasema Mbunge mwenye swali lake la mwanzo ataruhusiwa kuuliza maswali mawili tu ya nyongeza, Mbunge mwingine yeyote atauliza moja tu. Kwa hiyo c ya maswali yako original yalijibiwa, haya ya nyongeza basi ni mawili tu, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika naomba nimjibu Mheshimiwa Kilufi maswali yake mawili ya nyongeza. Hilo la tatu tutapata muda peke yetu kama ifuatavyo:-

Kwanza kuhusu shamba la NAFCO Mbarali analolizungumzia, shamba hili lilikwisha binafsishwa na shamba hili sasa hivi linamilikiwa na kampuni ya Highland Estates tangu Septemba, 2006.

Kwa utaratibu wa kubinafsisha mashamba lazima kuna utaratibu ambao tumekwisha kubaliana, tunachokifanya hivi sasa ni kwamba yule ambae anatumia shamba hilo, tunaangalia uwiano mzuri jinsi anavyoshirikiana na wakulima wanaomzunguka. Kunapotokea mgogoro kati ya yeye na wale wanaomzunguka basi kazi yetu ni kwenda kuangalia mgogoro ni upi na tutausaihishaje.

Hivi tunavyozungumza ni kwamba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amepanga ziara kama sikosei anakwenda kule baada ya Bunge hili kutembelea shamba hili kutizama kama kuna mogogoro mingine ambayo tunaweza tukaisuluhisha, tuweze kuisuluisha kwa

hiyo, naamini kabisa kwamba matatizo haya yatakwisha kati ya huyo mwenye shamba na wakulima.

Kuhusu swali  la pili, naomba labda nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba ntashirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, tutakwenda tulitizame vizuri suala hili la mipaka maana haliko tu kwake, inaonekana ili la kuingiliana mambo ya kilimo na hifadhi liko katika maeneo mengi hata kule Tabora nimeyaona yametokea na mahali pengine pengi.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba tutalishughulikia sisi kwa pamoja Wizara yangu na Wizara ya Maliasili na Utalii ili hatimaye tuweze kujua mipaka ni ipi na wananchi wajue mipaka yao wasiingiliane na sehemu za hifadhi.

Na.  7

**Ujenzi  wa  Barabara ya Tandale - Lupila - Mlangali**

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE** aliuliza:-

Barabara  ya Tandala-Lupila-Mlangali (Ludewa) yenye urefu wa km 60 ni miongoni mwa barabara zilizopandishwa hadhi na kuwa barabara ya Mkoa.  Barabara  hii ikijengwa itawezesha Mikoa mitatu ya Mbeya,Njombe na Ruvuma kuunganisha,yaani Isonje-Kitulo-Makete-Lupila-Mlangali Songea:-

Je, ni lini ujenzi  wa barabra hiyo utaanza?

**NAIBU  WAZIRI  WA  UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt.Binilith Satano Mahenge,Mbunge wa Makete,  kama ifuatavyo:-

Ni kweli barabara ya Tandala (Ikonda) - Lupila-Mlangali yenye urefu wa km 60 ni kati ya barabara zilizopandishwa daraja mwaka 2009 kutoka barabara ya Wilaya na kuwa barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa ujenzi wa barabara ya Tandala-Mlangali kwa kiwango cha changarawe tayari umeanza. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, jumla ya shilingi milioni 57 zilitumika kufanya matengenezo ya sehemu korofi kati ya Ikonda na daraja la Igangala. Matengenezo haya yamewezesha sehemu ya barabara kati ya Ikonda na Lupila kupitika.

Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ili barabara hii iweze kupitika kirahisi.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi kuishukuru sana Wizara ya Ujenzi, Waziri wake na Naibu Waziri kwa namna ya pekee wanavyosimamia ujenzi wa barabara na hususan katika Jimbo la Makete. (*Makofi*)

Kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana katika kukuza uchumi na hasa katika eneo hili la *Mtwara Corridor* ukizingatia kwamba barabara hii ni fupi na hivyo itawawezesha wananchi wa Mikoa ya Rukwa, Mbeya kwenda Ruvuma bila kupitia Makambaku na pia ukizingatia kwamba barabara hii inapita kwenye miradi mikubwa ya Taifa ikiwemo *Kitulo National Park,* shamba la ng'ombe la Kitulo na mradi wa Liganga.

(a)Serikali itatoa kipao mbele gani kuona kwamba kipande hiki cha kilometa 60 kinajengwa ili kuunganisha Mikoa hii niliyoisema?

(b)Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufika *site* na kuitembelea barabara hii ili impe nafasi ya kuweza kufanya maamuzi ya kuijenga kwa haraka zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Benelith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwanza Wizara inapokea pongezi zake, tunashukuru na pili Serikali inatambua kabisa umuhimu wa barabara hii kimawasiliano kwani inaondoa ulazima wa mtu kupitia Makambaku anayetokea Mbeya kwenda Njombe au kwenda Makete au kutoka Makete, Songea kuja Mbeya au Rukwa na ndiyo sababu tulikubali kuipandisha barabara hii daraja.

Mheshimiwa Spika, tuna mpango wa kukarabati barabara hii zaidi kwa sababu tunatambua vilevile kwamba kuna daraja muhimu katika barabara hiyo ya Mabangula ambalo limevunjika na tumeweka mpango katika mwaka ujao wa fedha kulitengeza hilo daraja na vilevile barabra hii kuikarabati na gharama za kazi hizo zimezingatiwa katika mapendekezo ya Bajeti ya Wizara tutakayowasilisha hapa na ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Mahenge pamoja na Wabunge wengine watatuunga mkono muda ukifika.

Mheshimiwa Spika, vilevile tuko tayari Wizara ya Ujenzi kuongozana na Mheshimiwa Mahenge kulitembelea eneo hili, ili kuweza kuweka msisitizo katika ukarabati wake, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tatizo ya barabara ya Tandala hadi Songea Ludewa huko linafanana na barabara ya Kibiti-Lindi ambayo ni adhabu kubwa katika Mikoa ya Kusini, ikiisha barabra ile itaonganisha Mikoa

ya Pwani, Lindi na Mtwara pia Tanzania, Msumbiji na Malawi. Ni lini itaisha tuna adhabu kubwa Kibiti-Lindi? Ahsante sana.

**SPIKA**: Yanafanana kwa sababu zote ni kilomita 60. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Mikidadi, mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara anayoiongelea pamoja na barabara nyingi, tungeomba Waheshimiwa Wabunge watuvumilie waje waangalie mapendekezo yetu katika Bajeti tutakayowasilisha. Nina hakika Mheshimiwa Fatma Mikidadi ataridhika na yale ambayo tumependekeza.

**SPIKA**: Wana *warm up,* tunaendelea na swali linalofuatia Waheshimiwa Wabunge kama alivyosema mtayasikia mengi katika Bajeti zao, Mheshimiwa Paulina Gekul.

Na. 8

**Nyumba zilizoathirika na Ulipuaji Miamba Katika Barabara ya Babati - Maisaka**

**MHE. CRISTOWAJA G. MTINDA (K.n.y. MHE. PAULINE GEKUL)** aliuliza:-

Ujenzi wa barabara ya kutoka Minjingu kwenda Singida umehusisha ulipuaji baruti kuvunja miamba ambao umeathiri nyumba za wananchi wa Babati Maisaka:-

Je, Serikali inawaambia nini wakazi wa Babati Maisaka ambao nyumba zao zimeathiriwa na milipuko ya baruti nzito ya kupasua miamba kupisha ujenzi wa barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paulina Gekul, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa yapo malalamiko ya baadhi ya wananchi wa kitongoji cha Maisaka "B" Mjini Babati kuhusu nyumba zao kuathiriwa na milipuko ya baruti inayofanywa na Mkandarasi wa sehemu ya barabara ya Dareda-Babati-Minjingu. Ulipuaji wa miamba katika eneo la Kilima cha Mruki ni kwa ajili ya kuzalisha kokoto zinazotumika katika ujenzi wa barabara.

Wakati wa maandalizi ya eneo hili wananchi waliokuwa karibu sana na mgodi wa kulipua na kuzalisha kokoto katika kilima cha Mruki nyumba zao zilifanyiwa tathmini na kulipwa fidia na wakahama kwenda maeneo mengine mbali na hayo hapo juu. Jumla ya shilingi milioni 405.601 zilitumika.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mkandarasi kuanza kazi ya ulipuaji miamba, Wananchi wengine wanaoishi kuzunguka mlima Mruki walitoa malalamiko ya nyumba zao kuathiriwa na milipuko hiyo.

Serikali iliamuru Mkandarasi kusimamisha kazi ya ulipuaji nyumba zote zenye malalamiko ili kubaini kama kweli zimeathirika na milipuko na kufanyiwa tathmini ya fidia.

Katika noezi hilo, nyumba zipatazo 52 zilibainika kuwa kweli zimeathirika na milipuko na Mkandarasi akawalipa jumla ya shilingi milioni 78. Aidha, walalamikaji 15 ambao tayari walikuwa wamefungua kesi mahakamani hawakuweza kulipwa fidia zao hadi hapo kesi itakapotolewa hukumu.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, nina swali la nyongeza. Kwa kuwa masuala ya ujenzi wa barabara zetu yanafanana katika nchi nzima na kwa kuwa wote tunafahamu kwamba barabara ya kutoka Manyoni-Singida imekwishakamilika na imeshafunguliwa na hivyo tunagemea kwamba mkandarasi awe ameshakamilisha shughuli zake na kuondoka.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba mkandarasi huyo wa Kichina ambaye alikuwa anajenga barabara ya kutoka Manyoni mpaka Singida bado yupo na ameanzisha shughuli nyingine ya uchimbaji wa kokoto katika kijiji cha Utaho, Tarafa ya Ihanja?

(b) Serikali inatuambia nini kuhusu mkataba mpya wa mkandarasi huyu wa kuanza shughuli nyingine ya kuchimba kokoto na ni lini mkataba huo umeingiwa na unaisha lini bila wananchi wa eneo husika kufahamishwa?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kwa niaba ya Serikali.

Lakini nimjibu pia Mheshimiwa Mbunge swali lake la nyongeza, swali la msingi lilikuwa ni ulipuaji wa kokoto katika barabara ya kutoka Manyoni kwenda Babati. Lakini swali lililoletwa na Mheshimiwa Mbunge ni la barabara ya kutoka Singida hadi Manyoni. Jibu lenyewe la msingi ni kwamba kandarasi anapomaliza kazi huwa anapewa muda wa mwaka mmoja hadi miaka mitatu kukaa kwenye *site* kufanya marekebisho ya yale yanayojitokeza.

Kwa hiyo wakati wa marekebisho pale bado ataendelea kuchimba kokoto na mahali panapomoka barabara analazimika mkandarasi kwa mujibu wa Sheria kuparudia na kupatengeneza. Kwa mkandarasi yule aliyemaliza barabara ya kutoka Singida hadi Manyoni ataendelea kukaa kwenye *site* mpaka zaidi ya mwaka mmoja.

Kwa hiyo asishangae kumwona kule na ataendelea kuchimba kokoto kwa ajili ya kufanya *rehabilitation* ya barabara. *(Makofi)*

Na. 9

**Posho ya Uhamisho kwa Askari Polisi**

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU (K.n.y. MHE. JOHN P. LWANJI)** aliuliza:-

Askari polisi wengi bado wanalalamika juu ya kuchelewa kulipwa posho zao za uhamisho:-

(a) Je, ni lini Serikali italimaliza tatizo hilo kwa kuwalipa askari hao malimbikizo ya posho zao za uhamisho?

(b) Kwa nini watumishi wengine wa Serikali wanapohamishwa hulipwa kwanza malipo hayo lakini kwa askari hutakiwa kutekeleza amri ya kuhama kwanza halafu malipo baadaye?

(c) Je Serikali haioni kuwa kwa kufanya hivyo inawaonea askari hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kulipa malimbikizo ya posho za uhamisho wa askari hadi kufikia mwezi Juni, 2012. Hivi sasa Wizara inaendelea kuiomba Wizara ya Fedha itupatie fedha hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, fedha za posho kwa ajili ya skari wakati wa uhamisho hutengwa katika Bajeti ya Serikali kwenye fungu la matumizi mengineyo *(other charges).* Kutokana na uhaba wa fedha inakuwa ni vigumu kuwapatia malipo askari wote waliopewa uhamisho.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli utaratibu huu si mzuri na unapunguza morali kwa askari. Ili kurekebisha hali hii, jeshi la polisi lipo katika mpango wa kuboresha utendaji wa jeshi la polisi.

Sehemu ya maboresho hayo inahusisha umuhimu wa kuzingatia maslahi ya askari na kuweka mifumo ambayo haitaruhusu askari kuhama bila kulipwa fedha zao za posho. Hata hivyo, jambo hili linahitaji uhakika wa kuwepo fedha za kudhibiti mahitaji ya dharura na hivyo kutoathiri fedha za posho za askari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nchemba ndiyo aliuliza swali hilo.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Aidha ninashukuru kwa majibu mazuri ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa uhamisho ni sehemu ya masharti ya kazi na posho ni haki ya mfanyakazi na kwa kuwa katika jibu la msingi ameelezea kwamba kutakuwepo na mfumo ambao hautaruhusu askari kuhama bila kulipwa fedha zao za posho.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akasema ni lini utaratibu huu utaanza ili kurudisha morali ya askari wetu hasa katika kufanya kazi na kudhibiti tishio la upotevu wa mali za wananchi hasa wakati wa maandamano? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba utaratibu huu si nzuri na ndivyo nilivyosema katika jibu langu la msingi na ndiyo maana nasema kwamba utaratibu tunautazama na tutakwenda katika njia mpya kabisa. Sasa anataka kujua lini utaratibu huu utaanza.

Niliombe Bunge lako Tukufu litupitishie Bajeti yetu atakayoisoma Mheshimiwa Waziri hapa na mle ndani upo utaratibu na nipende kushukuru kwamba tayari Sera ya Maboresho upande wa askari wa miaka 10 umeshapitishwa katika ngazi ya Serikali na humo humo ndipo utaratibu nzima ulimo.

Kwa hiyo niombe tu itakapokuja katika Bajeti mtayasikia baadhi ya majambo hapo mkishatupitishia nimhakikishie tu kwamba tutakapoanza Bajeti mpya na utaratibu mpya utatumika.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri ya Alu Habibi, Alhaj, Naibu Waziri Kagasheki, lakini naingia na wasiwasi na majibu yake.

Kwa kuwa Serikali ilikwisha toa ahadi kwamba askari hawa watalipwa malimbikizo yao ya madeni ya posho ya likizo na uhamisho. Hadi mwezi wa Juni mwaka huu kabla ya Bajeti itakayosomwa kesho na bado hawajalipwa wanawaongezea muda tena wa mwaka mmoja hadi mwakani.

Je, Serikali itatoa kauli gani nzito kupitia Wizara hii kuondosha tatizo la madeni ambayo ni usumbufu kwa askari wetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru yeye binafsi kwamba amekuwa mfuatiliaji wa suala hili lakini kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Edward Lowassa. Wamekuwa kwa kweli katika kikao kilichopita wametusaidia sana na hili limekuwa ni suala mojawapo ambalo wamelipa msukumo.

Sasa nimwambie kwamba azma ya Wizara na msimamo wa Serikali ni kwamba si vema kwamba madeni haya ya askari ambayo amekuwepo kwa muda mrefu yaendelee kuwepo. Hizi ni stahiki zao hizi, ni haki zao.

Agizo limekuwepo na hivi tuko katika mazungumzo na Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha imekubali kwamba haya madeni ambayo yamekuwepo mpaka kipindi cha mwaka wa fedha huu ambao tunaumaliza mwezi Juni yaishe na hayo yatakuwa ni yale ambayo yamekwishahakikiwa na ni madeni ya uhakika.

Kwa hiyo, niombe nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada zake na mapenzi makubwa aliyokuwa nayo kwa askari wetu na nimwambie kwamba hili tutalitekeleza, hapana wasiwasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Waziri wa Fedha, sasa akisimama Waziri wa Fedha unafanyaje, lazima ukubali tu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba niongezee majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nataka nikuhakikishie kwamba Serikali imeshaamua kwamba malimbikizo yote siyo ya Polisi peke yake, ya vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama yatalipwa kabla ya tarehe 30 mwezi huu. *(Makofi)*

Na. 10

**Kero Zinazowakabili Askari**

**MHE. MBAROUK SALIM ALI** aliuliza:-

Serikali inafanya jitihada za kuboresha makazi ya askari kupunguza kero ya makazi:-

(a) Je, ni lini askari watahamia katika jengo lao lililoko Limbani Wete?

(b) Serikali ina mpango gani wa kuongeza majengo katika eneo hilo ambalo bado lina nafasi ili kuboresha makazi ya askari wetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tayari askari wetu wameshahamia katika jengo analozungumzia Mheshimiwa Mbunge tangu mwezi Januari, 2011.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kujenga majengo mengine ya kuishi askari katika eneo hilo hilo na maeneo mengine nchi nzima kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini pia nashukuru kwa hatua za Wizara za kuboresha makazi ya askari wetu. Lakini pamoja na majibu hayo nilikuwa na swali moja la nyongeza. Kero ya makazi kwa askari polisi ni tatizo la muda mrefu, ni tatizo sugu na ni tatizo ambalo linaonekana kuendelea kwa sababu ya ajira ambazo zinafanyika karibu kila mwaka. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akatueleza ni askari wangapi kwa sasa bado wanaishi uraiani? Asante sana.

**SPIKA:** Haya! Hilo swali bwana, labda tumwone labda hodari, sasa sijui.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hakika siwezi nikakutamkia hapa kwamba ni askari wangapi lakini bado baadhi wanaishi uraiani. Isipokuwa kitu kimoja Mheshimiwa Mbunge nataka nikuambie, hili limekuwa ni tatizo la muda mrefu kama wewe mwenyewe ulivyotamka na wale ambao watakumbuka watajua kwamba awamu zote ambazo zimepita hili suala la makazi ya askari na nyinyi kama Waheshimiwa Wabunge katika maeneo mnayotoka mnajua kwamba hakuna jitihada kwa mrefu sana. Lakini katika awamu hii kwa kweli jitihada zinafanyika na nyumba zinaonekana na tumeweka msimamo na maamuzi kwamba askari wote lazima wapate makazi kama tulivyokuwa kule zamani kutakuwa na makazi ambayo wanakaa askari ili tuweze kuondokana na adha ya askari kuwa wanakaa uraiani. Kwa hiyo, nikujibu kwamba siwezi nikakupa idadi hapa lakini ni jambo ambalo sisi wenyewe linatutaabisha.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, Alhaj Kagasheki swali moja. Pamoja na kazi nzuri wanayofanya Wizara ya Mambo ya Ndani kuwajengea askari nyumba, labda nizungumzie zaidi upande wa Zanzibar. Yale maeneo ambayo sasa hivi baadhi ya askari wengi wanaishi ni zile nyumba za zamani ni mbovu na zinatisha sana. Sasa pamoja na suala la kuwajengea nyumba mpya ambazo huwa ni mbili au tatu ambazo zinachukua familia 12 mpaka 15 si zaidi ya hivyo.

Je, wana mpango gani madhubuti wa kuboresha zile nyumba ambazo ni za zamani lakini zinakalika zikifanyiwa marekebisho ili kupunguza hii dhiki ya askari, kwa sababu unajenga nyumba mbili lakini wanaoingia ni kidogo tu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Mhesihmiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alikuwepo Zanzibar na katika mazungumzo na katika kutazama hali halisi hili lilikuwa ni jambo ambalo limekuwepo.

Suala la maboresho pia zimo, yamo matatizo ya nyumba, ukarabati wa nyumba upande mmoja, lakini pia kujenga makazi mapya kwa askari kwa upande mwingine. Kwa vyovyote vile nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwmaba upande wa Serikali na upande wa Wizara azma tunayo na tunaona matatizo ambayo askari wetu wanakuwa nayo. Lakini kinachotukwaza hapa imekuwa ni suala la Bajeti.

Lakini nishukuru kwamba kumekuwepo na mazungumzo mazuri kati yetu sisi na Waziri wa Fedha lakini pia Kamati yako ambayo wewe ni Mjumbe kupitia Mwenyekiti wake mmekuwa mnafanya kazi kubwa katika kulisukuma hili na nina uhakika huko tunakokwenda siyo Zanzibar tu lakini pia Tanzania nzima tutaweza kuimarisha makazi ya askari wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Kama mtakavyotambua kipindi cha Bajeti, maswali yanakuwa 10 tu. Kwa hiyo tunatumia saa moja tu. Kipindi ambacho siyo cha Bajeti ndiyo tunakuwa na maswali 15 kwa maana ya kwamba tunakuwa na saa moja na nusu. Kwa hiyo tumeanza kipindi cha Bajeti ndiyo maana maswali yamekuwa 10 tu. Baada ya kusema hayo nina matangazo machache.

Tangazo la kwanza ni kwamba leo baada ya Maswali, sasa hivi baada ya Kuahirisha kikao cha Bunge, Waheshimiwa Wabunge naomba muende katika Ukumbi wa Msekwa tukafanye *briefing* tunayofanya kama kawaida ambayo tulitakiwa kufanya jana. Sasa jana tuligundua kwamba watu wengi walikuwa bado hawajafika, kwa hiyo tunafanya asubuhi hii. Tukitoka hapa mnakwenda kule katika Ukumbi wa Msekwa.

Lakini leo hii tena jioni saa 10 katika Ukumbi wa *St. Gasper*, Mheshimiwa Rais anataka kuwasilisha kazi ambayo Tume aliyoiunda imeifanya ya kuandaa Mpango. Anawasilisha kwa wananchi na kuwaeleza wananchi mapendekezo ya Tume ambapo hiyo hafla itafanyika kule *St. Gasper* saa kumi jioni.

Kwa hiyo, watu waliopewa mwaliko wawe wameketi saa tisa (9). Kwa hiyo, waliopewa mwaliko, nadhani nyinyi Wabunge ni wote, lakini na wananchi wengine wamepewa mwaliko.

Kwa hiyo, wawe wamekaa katika Ukumbi ule saa tisa (9) alasiri. Kwa hiyo ni Wabunge wote na wananchi walioalikwa.

Lakini pia Waheshimiwa Wabunge mnajua hapa tutakuwa na kipindi kirefu kukaa hapa Bungeni. Naomba niwakumbushe wale ambao hawajaandika majina yao kwa kalamu pale wanapotaka kukaa wafanye hivyo. Nadhani mpaka Jumatatu mtakuwa mmekamilisha. Inakuwa rahisi kwa sisi tunaokaa hapa Mezani kujua nani yuko wapi.

Kwa hiyo kama wapo wale ambao hawajakamilisha wafanye hivyo. Natambua wengine wamefanya, lakini wengine hawajafanya. Kwa hiyo, tujipe mpaka siku ya Jumatatu muwe tayari mmefanya hivyo. Kusudi tulete sasa vibandiko vile vyenyewe hasa vya chuma ambavyo vikiwekwa basi tena hapo unapotaka kukaa ni hapo hapo. Kwa hiyo, uwe na uhakika ndipo hapo unapotaka.

Sasa msije tena mkaanza mwingine anaingia mle anakaa kwenye kiti cha mwenzie. Kwa sisi Mezani mkikaa pale pale inatusaidia kuwafahamu mapema zaidi kuliko mkihama leo unahamia huko. Kwa hiyo ni mategemeo yetu kwamba mtakuwa mmefanya uamuzi huo.

Halafu naona tuna wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ushirika na Masoko kilichoko Moshi hapa wakiongozwa na Bi. Mary Kassim Kasimiri. Karibuni katika Ukumbi wetu na nadhani kesho ndio tunasoma Bajeti yetu kuanzia asubuhi saa 3 itakuwa kipindi cha maswali baada ya hapo Waziri wa Fedha atasoma Taarifa ya Hali ya Uchumi, halafu saa kumi jioni Bajeti. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge kesho asubuhi ni Hali ya Uchumi halafu jioni tutakuwa na Bajeti saa kumi jioni. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wote walionisaidia katika matatizo yangu ya msiba wa Mama yangu Mpendwa, ambao ulitokea tarehe 5 mwezi wa Mei. Nawashukuru sana kwa ushirikiano mliotupa ndani ya familia yetu. Tulifarijika sana. *(Makofi)*

Hatuna cha kuwalipeni isipokuwa Mungu awarudishie yale yote mema mliyotutendea. Ahsante sana. Baada ya kueleza hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 4.15 asubuhi Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano, tarehe 8 Juni, 2010 Saa Tatu Asubuhi)*